

UNA HERI WEWE ULIYESADIKI

Fidelis Kashumba

U na he ri (we we) we we u li ye sa di ki, kwa ma a na ya

ta ti mi zwa u li yo a mbi wa na Bwa na A le lu ya.

1. Mo yo wa ngu wa mwa dhi mi sha Bwa na na ro ho ya ngu

i me m sha - ngi li a, Mu ngu, Mwo ko zi wa - ngu.

2. Kwa kuwa Bwana ameutazama, kautazama, unyonge, wa mjakazi wake, mjakazi wake.
3. Kwa maana wewe na utazame, tokea sasa, vizazi wataniita, mimi, ni mbarikiwa.
4. Kwani mwenye nguvu kanitendea, kanitendea, ametenda makuu, nalo jina tukufu.
5. Na Rehema zake Bwana zadumu, nazo hudumu, vizazi na vizazi, kwao, wanaomcha.
6. Amefanya nguvu kwa mkono wake, kawatawanya, walio na kiburi, kwenye, mawazo yao.